

Kusimamia ugonjwa katika shule na huduma za watoto wadogo

Mojawapo ya mambo muhimu sana tunayoweza kufanya ili kupunguza kuenea kwa virusi vya korona (COVID-19) katika jamii yetu ni kukaa nyumbani wakati unapoumwa, hata kama tuna dalili ndogo sana.

Unahataji kujua hivi

Ikiwa mtoto anaumwa, hata na dalili ndogo sana, anapaswa kukaa nyumbani

Ikiwa mtoto anakuwa mgonjwa wakati wa siku, anapaswa kuchukuliwa kutoka shule/elimu na utunzaji wa watoto wadogo (ECEC) haraka iwezekanavyo.

Ikiwa mtoto ana dalili zozote za virusi vya korona (COVID-19) ambazo zinaelezea chini, hata ikiwa ni ndogo, anapaswa kupimwa na kukaa nyumbani mpaka amepokea majibu yake:

- homa
- homa ya baridi au kutoa jasho nyingi
- kikohozi
- maumivu ya koo
- upungufu wa pumzi
- pua yenye makamasi
- kupoteza uwezo wa harafu au ladha.

Katika hali fulani, kuumwa kichwani, kuumwa misuli, pua iliyojaa, kichefuchefu, kutapika, na kuharaisha zinaweza pia kufikiria kuwa dalili.

Ili kupata ushauri zaidi:

- piga simu kwa simu ya haraka ya masaa- 24 ya virusi vya korona (COVID-19) kwenye 1800 675 398
- piga simu daktari wako
- tumia [kifaa cha kujitathmini mtanadaoni](#) ya Idara ya Afya (Department of Health - DHS).

Tembelea: [Kupimwa wapi](#).

Mtoto anapaswa kukaa nyumbani hadi hana dalili zozote, hata kama kipimo chake cha virusi vya korona (COVID-19) kina jibu la hasi

Ikiwa mtu amepimwa chanya kwa virusi vya korona (COVID-19) au ametambuliwa kuwa mtu wa mawasiliano ya karibu anapaswa kujitenga /karantini hadi anapokea kibali kutoka DHS.

Watoto wenye dalili zinazoendelea kwa sababu ya hali ya msingi kama vile homa ya nyasi au pumu ambayo dalili zao ni kawaida kabisa za hali yao ndipo wanaweza kuendelea kuhudhuria ECEC/shule. Wanapaswa kupimwa kwa COVID-19 ikiwa wataanza kupata dalili ambazo ni tofauti au mbaya zaidi kuliko dalili zao za kawaida. Wanapaswa kufikiria kupata cheti cha matibabu kutoka kwa daktari wao ili kuhudhuria ECEC/shule ikiwa wana dalili zinazoendelea ambazo zinaweza kulingana na dalili za COVID-19 kama kikohozi au pua yenye makamasi.

Watoto wadogo (wa chekechea hadi Darasa la 2) wanaweza kuwa na dalili za muda mrefu baada ya kuumwa na virusi ya kawaida kama vile pua yenye makamasi au kikohozi na anaweza kurudi shuleni/ECEC kufuatia jibu la hasi la kipimo cha COVID-19 hata ikiwa bado wana dalili ndogo tu. Watahitaji cheti cha matibabu kutoka kwa daktari wao ili kuthibitisha kuwa wako wazima au wameponya kutoka ugonjwa wao mkali.

Kwa maelezo juu ya vipindi vya chini ambavyo wanafunzi na watoto wanavyohitaji kukaa nyumbani kwa hali nyingine, angalia [ratiba ya kutengwa shuleni ya DHS](#).

Watoto HAWAHITAJI cheti cha matibabu kabla ya kurudi shuleni/ECEC

Wakati dalili zimeondolewa, hakuna mahitaji kutoka Idara ya Elimu na Mafunzo (Department of Education and Training) au DHS kwa watoto/wanafunzi kuwa na cheti cha matibabu kabla ya kurudi shuleni/ECEC.

[Asante kwa msaada wako msaada wako katika kufuata hatua hizi, sisi pamoja tunaweza kukaa salama.](#)

Ushauri huu umeandaliwa na Idara ya Elimu na Mafunzo (Department of Education and Training), Utunzaji wa Salama Zaidi wa Victoria (Safer Care Victoria) na Idara ya Afya (Department of Health)